TANGAZO LA SERIKALI NA. 870 la tarehe 1/12/2023

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA WA MAGARI MANNE YANAYOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA AFYA KWA AJILI YA MRADI WA USIMAMIZI WA AFYA YA MWAKA, 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa wa magari manne yanayoingizwa nchini na Wizara ya Afya kwa ajili ya Mradi wa Usimamizi wa Afya ya Mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tarehe 3 Novemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa magari manne yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii yaliyoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa nchini kabla ya kibali cha forodha yatatumika na Wizara ya Afya kwa ajili ya mradi wa usimamizi wa afya - Global Fund unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa gari tajwa litatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine

ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 1 Mei, 2023.

———

JEDWALI

———

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1. | LANDCRUISER 76 HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS. | JTEEB71JX0F023522 | 1HZ - 1033539 |
| 2. | LANDCRUISER 76 HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J90F023527 | 1HZ - 1033551 |
| 3. | LANDCRUISER PRADO TXL TURBODIESEL, 5 DOORS, 7-SEATER | JTEBRFJ70K303022 | 1GD - 9130406 |
| 4. | LANDCRUISER 76 HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J50F025498 | 1HZ - 1044403 |

Dodoma,
21 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha.*